

Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara Kuhusu Mgawanyo wa Hisa wa NMB

1. *Hisa ni Nini?*

Hisa ni sehemu ya umiliki katika kampuni. Kampuni huuza sehemu au hisa zote za umiliki wake kwa wawekezaji ili kukusanya mtaji. Wawekezaji wanaomiliki hisa za kampuni hujulikana kama Wanahisa. Wamiliki wa hisa hupata faida kutokana na uwekezaji wao kupitia gawio na pale ambapo kuna ongezeko la thamani ya hisa.

2. *Gawio ni nini?*

Gawio ni Malipo kwa wanahisa yanayotokana na sehemu ya faida halisi baada ya kodi ya kampuni. Malipo haya yanapendekezwa na wakurugenzi wa kampuni na kuthibitishwa na Wanahisa katika mkutano mkuu. Gawio linaweza kulipwa kama pesa taslimu au kwa kuongeza hisa kwa wanahisa.

3. *Soko la hisa la Dar-es-Salaam ni nini?*

DSE ni kifupi cha Dar es Salaam Stock Exchange, Soko la Hisa ni soko ambalo huwezesha hisa, hatifungani na dhamana zingine zilizoordheshwa katika soko hilo kuuzwa na kununuliwa.

4. *CSDR ni nini?*

CSD & Registry Company Limited (CSDR) ni kampuni tanzu ya DSE iliyoidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya mitaji na Dhamana (CMSA) kuhifadhi kumbukumbu za umiliki wa dhamana kama vile Hisa pamoja na Hatifungani zinazomilikiwa na watu binafsi au taasisi.

5. *Akaunti ya CDS ni nini*

Akaunti" ya CDS ni mfumo wa kielektroniki unaotumika kuhifadhi kumbukumbu za umiliki wa dhamana kama vile Hisa pamoja na Hatifungani zinazomilikiwa na watu binafsi au taasisi. Mfumo huu unasimamiwa na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), unawawezesha wawekezaji kununua, kuuza, na kuhamisha dhamana.

6. *Mgawanyo wa Hisa wa NMB ni nini?*

Mgawanyo wa hisa ni tukio muhimu ambapo kila hisa ya kawaida ya NMB iliyotolewa na kulipiwa kikamilifu itagawanywa katika hisa kumi (10) za kawaida, Hivyo, kila hisa moja iliyopo itabadilika kuwa hisa kumi.

7. *Uwiano wa mgawanyo wa hisa ni upi?*

Uwiano wa mgawanyo ni 1:10, ikimaanisha kuwa kila hisa moja ya kawaida ya NMB itagawanywa na kuwa hisa kumi (10) za kawaida.

8. *Kwa nini Benki ya NMB inafanya mgawanyo wa hisa?*

Mgawanyo wa hisa unalenga kuongeza unafuu wa bei ya hisa za NMB, kuimarisha ukwasi wa hisa za benki ya NMB sokoni, pamoja na ushiriki mpana, hususani kwa wawekezaji wadogo katika soko la mitaji.

9. ***Je, mgawanyo wa hisa utabadilisha thamani ya uwekezaji wangu?***
Hapana. Mara tu baada ya mgawanyo, thamani ya uwekezaji wako hautabadilika kwa kuwa ongezeko la idadi ya hisa litafidiwa na kupungua kwa bei ya kila hisa kwa uwiano unaolingana.
10. ***Je, nitapokea hisa za ziada bila malipo?***
Ndiyo. Baada ya maboresho ya daftari la wanahisa, kila hisa moja (1) ya NMB itagawanywa kuwa hisa kumi (10), hivyo idadi ya hisa unazomiliki itaongezeka mara kumi.
11. ***Je, ninapaswa kulipia hisa hizo za ziada?***
Hapana. Hakuna mwanahisa atakayehitajika kufanya malipo yoyote.
12. ***Je, ninahitaji kujaza fomu zozote?***
Hapana. Hakuna mwanahisa atakayehitajika kuwasilisha fomu yoyote au nyaraka zozote.
13. ***Je, mgawanyo wa hisa unahusisha riba, mkopo au miamala ya kifedha yenye riba?***
Hapana. Mgawanyo wa hisa hauhusishi riba, ukopesaji, ukopaji au miamala ya kifedha yenye riba. Ni mabadiliko yanayoongeza idadi ya hisa zinazomilikiwa na wanahisa huku bei ya hisa ikipunguzwa kwa uwiano unaolingana bila kubadilisha thamani ya uwekezaji wao.
14. ***Nani anastahili kunufaika na mgawanyo wa hisa?***
Wanahisa wote watakaokuwepo katika daftari la wanahisa kufikia Ijumaa, tarehe 21 Agosti 2026 watapokea hisa kumi kwa kila hisa moja wanayomiliki.
15. ***Tarehe ya kufungwa daftari la wanahisa ni ipi?***
Ijumaa, tarehe 21 Agosti 2026.
16. ***Ni lini hisa zitaanza kuuzwa pamoja na stahiki ya mgawanyo wa hisa?***
Jumatatu, tarehe 27 Julai 2026.
17. ***Ni tarehe gani ya mwisho ambayo hisa zitauzwa pamoja na stahiki ya mgawanyo wa hisa?***
Jumatano, tarehe 19 Agosti 2026.
18. ***Je, Nikinunua hisa za NMB tarehe 19 Agosti 2026, nitastahili kupata mgawanyo wa hisa?***
Ndiyo. Ununuzi wowote wa hisa za NMB utakaofanyika tarehe 19 Agosti 2026 au kabla ya tarehe hiyo utampa mwekezaji stahiki ya kupata mgawanyo wa hisa.
19. ***Je, nikinunua hisa wakati shughuli za uuzaji na ununuzi wa hisa zimesimamishwa kwa muda, nitastahili kupata mgawanyo wa hisa?***
Hapana. Katika kipindi hicho hakutakuwa na ununuzi wala uuzaji wa hisa za Benki ya NMB hadi Jumatatu, tarehe 24 Agosti 2026.

20. ***Je, kutakuwa na kusimamishwa kwa muda shughuli za uuzaji na ununuzi wa hisa za NMB?***
Ndiyo. Shughuli za uuzaji na ununuzi wa hisa za Benki ya NMB zitasimamishwa kwa muda kuanzia Jumatano tarehe 19 Agosti 2026, saa 10:00 jioni mara baada ya soko kufungwa hadi Jumatatu, tarehe 24 Januari 2026, siku ambayo soko litafunguliwa tena rasmi.
21. ***Kwa nini shughuli za uuzaji na ununuzi wa hisa za NMB zitasimamishwa kwa muda?***
Kipindi hiki cha usimamishaji kimetengwa ili kutoa fursa kwa Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), CSDR, pamoja na Benki ya NMB, kufanya uhakiki na maboresho ya daftari la wanahisa, ili kuhakikisha kuwa kila hisa moja inayomilikiwa na mwanahisa inagawanywa na kuwa hisa kumi.
22. ***Shughuli za uuzaji na ununuzi wa hisa za NMB zitarejea lini baada ya kusimamishwa kwa muda?***
Shughuli za uuzaji na ununuzi wa hisa zitarejea mara baada ya soko kufunguliwa siku ya Jumatatu, tarehe 24 Agosti 2026.
23. ***Tarehe ya Utekelezaji rasmi wa mgawanyo wa hisa ni ipi?***
Jumatatu, tarehe 24 Agosti 2026.
24. ***Wanahisa wataona lini hisa zao zilizoongezwa kwenye akaunti zao?***
Baada ya kufanya uhakiki na maboresho ya daftari la wanahisa.
25. ***Nini kitatokea katika oda za NMB zitakazokuwa zimesalia kwenye mfumo wa soko la hisa baada ya soko kufungwa siku ya tarehe 19 Agosti 2026?***
Oda zote za kuuza na kununua hisa za NMB zitazokuwa zimesalia kwenye mfumo wa soko la hisa mara baada ya soko kufungwa tarehe 19 Agosti 2026 zitafikia ukomo wake mara moja. Wawekezaji ambao oda zao zitakuwa zimefikia ukomo wake wanashauriwa kuziweka tena oda hizo kupitia kwa mawakala wa soko la hisa au mifumo ya kidijitali ya soko mara baada ya soko kufunguliwa siku ya Jumatatu tarehe 24 Agosti 2026.
26. ***Ninawezaje kuwasilisha upya oda za NMB zilizofikia ukomo wa muda baada ya soko kufungwa Jumatano saa 10:00 jioni?***
Kupitia kwa mawakala wa soko la hisa au mifumo ya kidijitali ya soko mara baada ya soko kufunguliwa siku ya Jumatatu tarehe 24 Agosti 2026.
27. ***Nini kitatokea kwa bei ya soko baada ya mgawanyo wa hisa?***
Soko litakapofunguliwa tena Jumatatu, tarehe 24 Agosti 2026, bei ya hisa za NMB itafuata taratibu na miongozo ya soko la hisa zinazosimamia mgawanyo wa hisa.
28. ***Je, Thamani ya mtaji wa soko la hisa wa NMB Bank Plc utabadilika?***
Hapana. Mgawanyo wa hisa hautabadilisha thamani ya mtaji katika soko la hisa.

29. Je, mgawanyo wa hisa utaathiri umiliki wa hisa za NMB?

Hapana. Umiliki wa hisa zako hautabadilika kwa kuwa ongezeko la idadi ya hisa litafidiwa na kupungua kwa bei ya kila hisa kwa uwiano unaolingana.

30. Je, haki za mwanahisa za kupiga kura zitaathirika?

Hapana. Haki za mwanahisa za kupiga kura zitaendelea kuwa sawa na umiliki wako wa hisa.

31. Je, haki za kupokea gawio zitaathirika?

Hapana. Haki za kupokea gawio zitaendelea kuwa sawa na umiliki wako wa hisa.

32. Je, gawio la baadaye litazingatia idadi mpya ya hisa?

Ndiyo. Gawio la baadaye litazingatia idadi ya hisa utakazomiliki baada ya mgawanyo, pamoja na kiwango cha gawio kwa kila hisa kitakachotangazwa.

33. Itakuwaje ikiwa ninamiliki hisa moja tu?

Hisa hiyo moja itagawanywa na kuwa hisa kumi baada ya mgawanyo.

34. Je, mgawanyo wa hisa unamaanisha kampuni inatoa mtaji mpya?

Hapana. Mgawanyo wa hisa unaongeza tu idadi ya hisa na kupunguza bei kwa uwiano unaolingana.

35. Ninawezaje kuthibitisha umiliki wangu baada ya mgawanyo wa hisa?

Unaweza kuthibitisha umiliki wako kupitia kwa mawakala wa soko la hisa au mifumo ya kidijitali ya soko mara baada ya soko kufunguliwa siku ya Jumatatu tarehe 24 Agosti 2026.

36. Ninaweza kupata taarifa zaidi wapi?

Namba ya simu: **0800 002 002**

Ukiwa nje ya Tanzania: **0808 002 022**

Barua Pepe: tuambie@nmbbank.co.tz

Mifano ya Mgawanyo w hisa za Benki ya NMB

Idadi ya hisa Kabla ya Mgawanyo

1
10
50
100
500
1,000
5,000
10,000

Idadi ya Hisa Baada ya Mgawanyo

10
100
500
1,000
5,000
10,000
50,000
100,000